

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



Boma Road,
S.L.P. 484,
SINGIDA,
Barua Pepe: rbcsgivingida@pccb.go.tz.
TANZANIA.

www.pccb.go.tz

SINGIDA – APRILI 24, 2020

TAARIFA KWA UMMA

AFISA ELIMU ATIWA MBARONI AKIMHONGA AFISA TAKUKURU

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Singida inawashikilia Afisa Elimu Vifaa na Takwimu wa Halmashauri ya Wilaya ya IRAMBA Bw. ALBERT NGIMBA na Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi ISENENGWA Bw. GEORGE MMEMBWA kwa makosa ya kushawishi na kutoa hongo ya shs.Laki tano (500,000.00) kwa Afisa Uchunguzi wa TAKUKURU Wilaya ya IRAMBA (jina limehifadhiwa) kwa lengo la kumshawishi Afisa huyo awasaidie kwenye uchunguzi unaohusiana na tuhuma za ufujaji na ubadhirifu wa fedha zilizotolewa na Serikali Kuu kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za walimu na vyoo kwenye baadhi ya shule za msingi wilayani hapo.

Watuhumiwa hao walikamatwa na Maafisa wa TAKUKURU kwa kushirikiana na Maafisa wa Jeshi la Polisi tarehe 22/04/2020 majira ya saa nne usiku nyumbani kwa Afisa huyo wakiwa wamempelekea shs.Laki tano (500,000.00) kama sehemu ya shs. Milioni nne (4,000,000.00) waliyokuwa wamemuahidi.

Uchunguzi wa tuhuma hizi unaendelea na punde utakapokamilika watuhumiwa watafikishwa mahakamani kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007.

Aidha, uchunguzi wa tuhuma za ufujaji na ubadhirifu wa fedha kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za walimu na vyoo kwenye baadhi ya shule unaendelea na pindi utakapokamilika mtajulishwa.

TAKUKURU Mkoa wa Singida inatoa wito kwa wananchi wa Mkoa huu kuzidi kushirikiana kwa kutoa taarifa za vitendo vya rushwa na kufika mahakamani kutoa ushahidi wao pale itakapohitajika. Ofisi za TAKUKURU zipo kwenye Wilaya zote za Mkoa wa Singida.

Taarifa hii imetolewa na:

**ADILI ELINIPENDA
MKUU WA TAKUKURU (M)
SINGIDA**